

SHULE YA SEKONDARI

MTIHANI WA KISWAHILI KIDATO CHA TATU FEBRUARI 2019

MUDA: saa 2

MAELEKEZO

- Jibu maswali yote
- Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali
- Andika jina lako katika kila ukurasa wa karatasi yako ya majibu.
- Pigia mistari ya pambizo katika karatasi yako ya kujibia pande zote nne kwa ukubwa wa rula(juu,chini,kushoto na kulia)

SEHEMU A: UFAHAMU

1.Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Wapendwa wazazi wangu,

Leo ni siku ya nafuu kwa wafungwa vijana. Nimepewa robo saa ili niwakumbuke kwa barua. Nami bila ajizi nachukua fursa hii kwanza kuwaamkieni. Bila shaka wapendwa wazazi mnaikumbuka siku ile siku ya mechi ya kandanda baina ya shule yetu na ile shule iliyotoka kijijini

Basi ni kweli ndicho kiini.Ati sisi watoto wa kitovu cha jiji tufungwe goli saba na watu wakuja! kweli mimi pamoja na wenzangu wengi tulipandwa na jazba , japo hapakuwa na muafaka tangu awali wa kutenda tuliyotenda lakini tuliyatenda makosa maovu kweli! mwenyezi mungu atuhurumie.kumi walilala chini milele.

mpendwa baba yangu unakumbuka siku nilipotaja “pesa za shule” ulichomoa minoti bila ya kuhesabu. nilisema zinatakiwa “tuisheni” lakini zote ziliishia kwenye Unga wa kubwia na misokoto ya kuvuta. Isitoshe zingine zilinisaidia kuwanasa mapatna kwenye disko, hata wale walio mkaribia mama yangu kiumri.

mama unakumbuka siku ile ulipopita ubavuni mwa shule yetu kutoka sokoni? uliponikuta nimepiga magoti mbele ya walimu kwa kosa la kumpiga mwalimu? ulifanyeje? ukawalowesha walimu kwa matusi ya nguoni kisha ukaninyakua ukanitumbukiza ndani ya benzi lako na kuwaacha walimu wale wakifikicha macho kwa vumbi ulilowatimulia. Mama siku ile nilijiona kama malaika anayepaa

mbinguni! lakini hapa jela najiona kama mjusi aliyebanwa na jiwe! Tangu niingie hapa mwaka sasa nimeoga mara mbili, nimekula nikashiba mara moja, nimepigwa na manyapala mara mia, nimeua chawa milioni, nime,.....Ohooo huyooo, Afande anakuja na rungu.....majuto!

Maswali

- (i) Tukio gani lililomfanya majuto afungwe?
 - (ii) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari hii;
 - a) Kumi walilala chini milele
 - b) unga
 - c) misokoto
 - d) mapatna
 - e) kitovu cha jiji
 - (iii) Je, ni kwa vipi mama yake majuto anapaswa kulaumiwa kwa malezi ya majuto?
 - (iv) Je, unafikiri naye baba yake majuto tunapaswa kumlaumu kwa lipi?
 - (v) Taja methali moja inayoendana na kisa cha majuto
 - (vi) Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa habari hii.
2. Andika ufupisho wa habari hii kwa aya moja isiyozidi maneno 50 na isiyopungua maneno 25

SEHEMU B SARUFI

3. Kwa mifano bainisha miundo mitano ya kiima
4. Fafanua hatua tano muhimu anazotakiwa kuzifuata mtu anayechanganua sentensi
5. Vishazi tegemezi ni nini? kwa mifano fafanua aina mbili za vishazi tegemezi.
6. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi
Wanafunzi wakorofi wataadhibiwa kesho
7. Kwa mifano ya sentensi, taja ngeli za nomino zifuatazo
 - i) Mzazi
 - ii) Kinywaji
 - iii) Kulima

iv) Michele

v)Ugonjwa

SEHEMU C-UANDISHI

8. Andika insha isiyo pungua maneno 200 na isiyozidi maneno 300 kuhusu sababu za wanafunzi kutofanya vizuri kwenye mitihani ya taifa

9.Andika barua kwa mwajiri yoyote Yule uombe kazi ya ulinzi

SEHEMU D FASIHI KWA UJUMLA

10. Tunga ngonjera isiyopungua beti nne kuhusu tohara kwa wanawake.